

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

Telegramu: "LEGAL"

Simu Na.: +255 26 2310019

Nukushi: +255 26 2310056

Barua Pepe: [km@sheria.go.tz](mailto:km@sheria.go.tz)

Tovuti: [www.sheria.go.tz](http://www.sheria.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Katiba,  
S. L. P. 315,  
40484 DODOMA.

**T A N G A Z O K W A U M M A**

Kufuatia taarifa ya matokeo ya wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ya hivi karibuni, na baada ya kuibuka kwa tatariki mionganoni mwa wanajamii wakiwemo wanazuoni na wadau mbalimbali wa sekta ya sheria kuhusu ufaulu mdogo wa wanafunzi katika tasnia ya Sheria, tarehe 12 Oktoba, 2022 Mheshimiwa Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria aliunda Kamati Maalum ya kufanya tathmini ya mfumo wa elimu ya Sheria nchini na changamoto zinazoukabili mfumo huo ikiwa ni pamoja na namna mafunzo ya uanasheria kwa vitendo yanavyotolewa.

Pamoja na mambo mengine, Kamati hiyo imepewa jukumu la kushauri namna ya kuboresha mfumo huo ili kukidhi mahitaji ya taaluma ya Sheria kwa lengo la kuwa na ushindani wa kitaifa na kimataifa. Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Hadimu za Rejea ilizopewa, itapokea maoni kwa maandishi pia kuwasikiliza wadau mbalimbali ana kwa ana.

Kwa kuwa siyo wananchi wote watapata fursa ya kufika mbele ya Kamati kutoa maoni, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mwenyekiti wa Kamati anawaalika wananchi na wadau wenyewe mapenzi mema na uboreshaji wa mfumo wa elimu ya sheria nchini na elimu ya uanasheria kwa vitendo, kuwasilisha maoni kwa maandishi ili kuiwezesha Kamati kupata maoni mengi kadri inavyowezekana na hatimaye kushauri ipasavyo. Mwisho wa kupokea maoni ya maandishi ni tarehe 24 Oktoba, 2022 saa 10:00 jioni.

Maoni hayo yawasilishwe kuitia barua pepe ya [km@sheria.go.tz](mailto:km@sheria.go.tz), mitandao ya kijamii ya twitter: @Sheria\_Katiba; Instagram @katibanasheria\_ au WhatsApp kwa namba 0742 910529.

IMETOLEWA NA:  
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**  
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**  
**18 Oktoba, 2022**